SAMHSA
Substance Abuse and Mental Health Services Administration

New England (HHS Region 1)
PTTC Prevention Technology Transfer Center Network
Funded by Substance Abuse and Mental Health Services Administration

Bangi huko Marekani

Mwongozo wa Watu Wasio Raia katika jimbo la Maine

Umeundwa na Laurie Jevons, MS, PSC, PMP

Novemba 2021

Jedwali la Yaliyomo

Ukurasa wa 3	Matumizi ya Bangi Miongoni mwa Watu Wazima huko Maine
Ukurasa wa 4	Ufafanuzi wa Bangi pamoja na THC
Ukurasa wa 5	Kufafanua CBD, Hashi, & Sheria za Matumizi
Ukurasa wa 6	Ya Kimatibabu ya Vikorokoro na Taarifa ya
Ukurasa wa 7	Athari za Kiafya za Wale Wasio Raia
Ukurasa wa 8	Kufanya Kazi katika Kiwanda cha Bangi, ya Msaada wa Kifedha
Ukurasa wa 9	Marejeleo & Rasilimali
Ukurasa wa 10	Laha ya Uhalisia wa Mambo

Bidhaa hii imeundwa na Laurie Jevons chini ya Programu ya New England ya 2021 ya Ushirika wa Kituo cha Uhawilishaji Ulinzi wa Teknolojia (PTTC) New England PTTC na programu hii vinadhaminiwa na SAMHSA ya Idara ya Afya na Huduma za Binadamu ya Marekani (HHS). Yaliyomo ni yale ya mwandishi na sio lazima yawakilishe mitazamo rasmi ya, wala uungwaji mkono wa, na SAMHSA/HHS, ya Serikali ya Marekani.

Matumizi ya Bangi kwa raia wa kigeni yanaweza kusababisha kufurushwa kutoka Marekani.

Huku jimbo la Maine likiwa limehalalisha bangi kwa matumizi kwa mtu mzima, Marekani inazingatia bangi kama Dawa ya Ratiba ya 1, kuwa haramu chini ya sheria ya shirikisho. Kwa kuwa sheria ya serikali ya shirikisho inazidi sheria ya jimbo, watu wasio raia wanaweza kuadhibiwa kwa kutumia au kushughulikia bangi, ikiwa ni pamoja na hata kufanya kazi katika kiwanda cha bangi. Katika mwongozo huu, watu ambao sio raia inamaanisha mtu yeyote anayeishi, kufanya kazi, au kuingia Marekani bila ya uraia wa Marekani. Hii ni pamoja na wale walio na kadi ya green card (wakazi wa kudumu), wakimbizi na wanaotafuta ukimbizi, wahamiaji ambao hawajaorodheshwa rasmi, walio na hali nyinginezo (kama vile Hali Iliyocheleweshwa kwa Ajili ya Kufikia Utoto), sawa na Visa Maalum za Mhamiaji (SIV) kwa Watafsiri/Wakalimani wa Kiiraki na Kiafugani.

Jifunze Zaidi:

Mambo Wanayopaswa Kujua Wale Wasio Raia

Matumizi ya Bangi Miongoni Mwa Watu Wazima kwenye jimbo la Maine

Chini ya Sheria ya Maine ya Matumizi ya Bangi, watu wazima wenye umri wa zaidi ya miaka 21 wanaweza kununua, kupatikana, na kupanda bangi. Bangi ni halali kwa raia wa Marekani walio na umri wa zaidi ya miaka 21 kutumia au kupatikana nayo wakiwa katika jimbo la Maine, lakini si halali kusafirisha bangi katika majimbo mengine au katika mipaka ya kimataifa. Ni haramu kwa mtu yeyote kutumia bangi katika maeneo ya umma (ikiwa ni pamoja na kwenye bustani, njia za kutembelea na katika mikahawa). Inasalia kuwa haramu kwa mtu yeyote aliye na umri wa chini ya miaka 21 kupatikana na au kusafirisha bangi, hata katika jimbo la Maine.

Kuifafanua Bangi

Bangi[1] (inayojulikana pia kama marijuana, biri, ganja, majani,msokoto wa bangi,mitishamba, dawa sugu) ina viambajengo vingi vikiwemo THC (delta-9-tetrahydrocannabinol), CBD (cannabidiol),na mmea wa bangi.

Bangi inaweza kutumika kwa njia mbali mbali, ikiwa ni pamoja na:

- uvutaji (sigara, ganja, buruma,kiko)
- vilaji venye bangi (bidhaa zilizochanganywa)
- kuvuta na kutoa mvuke wenye nikotini
- kufyonza (nta iliyokozwa, shata, buda)

Ua/sigara zilizokolezwa

Vilaji venye bangi

Bidhaa

THC (delta-9-tetrahydrocannabinol)

THC ni kipengele cha bangi kinachobadilisha akili. THC husababisha furaha tele na utulivu, huongeza hisia na kubadilisha dhana ya muda. Kadhalika, THC huharibu maarifa ya uendeshaji gari, inaweza kusababisha mhemko au kuchanganyikiwa, na huvuruga utendakazi wa mapafu kutokana na uvutaji wa bangi wa mara kwa mara THC ndiyo kipengele amilifu cha bangi kilichogunduliwa katika vipimo vya dawa za kulevya. Kwa kutegemea viwango na idadi ya vipindi vya THC viliyotumika, chembechembe za THC zinaweza kusalia kwenye mwili kwa siku au wiki kadhaa.

"Ishara ya pamoja" inaonyesha bidhaa ina THC, na inaweza kuonyeshwa kwenye lawalawa/ vyakula, maua yenyewe ya mmea wa bangi, au bidhaa zilizokolezwa.

Kuifafanua Bangi *(inayoedelea)*

Hashishi (hashi)

Hashi ni miongoni mwa aina za bangi zilizokolea zaidi. Hashi inatolewa kwenye bangi safi (resini kavu) ya mmea wa bangi nakusindikwa ili kuwa mafuta, siagi, nta (vikolevu vya THC). Ukolevu wa THC katika ua la mmea wa bangi ni wa jumla ya 20%, lakini unaweza kuwa juu hadi 80% katika ukolevu.

CBD (cannabidiol)

CBD ni sehemu ya bangi isiyovuruga akili. CBD inaweza kutumika kutibu mihemko, ukosefu wa usingizi, na maumivu ya muda mrefu (kama baridi yabisi), ijapokuwa utafiti kuhusu athari za CBD ni kidogo. CBD inaweza kuongezwa kwenye mafuta ya losheni, jeli, majimaji, au kalamu za mvuke. Kwa kuwa hakuna sheria zinazosimamia bidhaa za CBD, inaweza kuwa vigumu kujua kiasi halisi cha CBD au THC kilichopo kwenye bidhaa.

Vikorokoro

Idara ya Haki ya Marekani inafafanua vikorokoro kama kifaa chochote kinachotumika kuzalisha, kuficha, au kutumia dawa za kulevya. Hii inaweza kujumuisha karatasi za misokoto, paipu, kiko, visagaji, au paipu za nta.

Ijapokuwa baadhi ya vikorokoro vinaweza kutumika kinyume cha sheria (kama vile tumbaku), utekelezaji wa sheria unaweza kupima bidhaa ili kuhakikisha ikiwa kuna mabaki ya bidhaa haramu. Ni kinyume cha sheria kwa wale wasio raia kutokubali kukaguliwa kwa mizigo yao, kama vile kumiliki vikorokoro huweza kusababisha kuongezeka kwa viwango vya uchunguzi.

Visagaji

Kalamu za mvuke

Matibabu ya Marijuana ya Maine

Chini ya Sheria ya Matibabu ya Marijuana ya Maine, wagonjwa walio na zaidi ya umri wa miaka 18 walio na kadi ya kitambulisho cha matibabu ya marijuana wanaweza kununua bangi kutoka kwa mtoa huduma aliyesajiliwa. Hata hivyo, katika shirikisho, bangi ni kinyume cha sheria na inaweza kusababisha hatari kwa wale wasio raia (hata kwa wale walio na kadi halali ya matibabu). **Ikiwa wewe sio raia na unahisi kwamba bangi ya matibabu ndio njia ya pekee ya kutibu dalili, ni muhimu kupata ushauri wa mwanasheria**. Kumbuka: kama mwenyeji wa Maine, haki zako hubadilika pindi tu unaposafiri nje ya jimbo la Maine. Kama mtu asiye raia, kadhalika haki zako hubadilika unaposafiri nje ya Marekani.

Athari za Kiafya za Kutumia Marijuana

Kutumia bangi kwa THC huathiri pakubwa akili na mafunzo, na huweza kuwa na athari shuleni ama kazini. Kadhalika THC huathiri vipindi vya kujibiza na kuharibu mawasiliano ya viungo pamoja na usawa wa ulinganifu wa mwili. Kwa kuwa uvutaji wa bangi una viwango vile vile vya kemikali kama tumbaku, wanaovuta wanaweza kukumbana na ugonjwa wa mapafu ama matatizo ya kupumua.[2]

Hakuna kiwango salama cha kutumia bangi hususan ukiwa na ujauzito ama kunyonyesha, kama THC inavyohusishwa na athari katika ukuaji wa mtoto. [3]

Jifunze Zaidi:

Vyema Kujua

Taarifa kwa Wasio Raia

Kituo cha Kisheria cha Masuala ya Wahamiaji kinapendekeza kujiepusha kutumia bangi kwa hali yoyote ile. Hii ni pamoja na:

- kupatikana na bangi au vikorokoro (karatasi za misokoto, paipu, visagaji) ukiwa nje ya nyumba
- kuchapisha picha zinazohusiana na bangi kwenye mtandao wa kijamii
- kuwa na picha au video za bangi kwenye simu yako
- ukiwa umevaa mavazi yaliyo na maneno au nembo ya bangi
- kuongea kuhusu matumizi au kupatikana kwa bangi na maafisa wa uhamiaji au mpaka[4]

Huko Marekani, watu wasio raia wana haki na afisa wa polisi na Watekelezaji wa Uhamiaji na Forodha (ICE). Hizi ni pamoja na **haki ya kuwa kimya,** pamoja na **haki ya kukataa ridhaa** ya mtu wako ama mali yako. Iwapo utaulizwa maswali na afisa wa uhamiaji au polisi kuhusu umiliki au matumizi yaliyopita ya bangi, usikubaliane na chochote kabla ya kupata ushauri wa mwanasheria.

Mahojiano ya uhamiaji yanaweza kuhusisha maswali kuhusu utumiaji, upatikanaji, au kuajiriwa katika kipindi kilichopita. Ikiwa hujatumia au kupatikana na bangi, unaweza kujibu la.
Ikiwa umetumia au kupatikana na bangi katika kipindi kilichopita, unaweza kukataa kujibu swali hilo na kuomba kuongea na wakili.

Jifunze Zaidi:
Fahamu Haki Zako

Uzingatifu Mwingine

Kudhibitishiwa Uraia

Watu wasio raia na ambao wamekubali kuwa wametumia au kufanya kazi katika sehemu za bangi wanaweza kunyimwa Udhibitishwaji wa Uraia kwa kukosa kile ambacho sheria za uhamiaji zinaita 'hulka ya maadili mema'. Serikali ya Marekani inazingatia upatikanaji wa bangi au vikorokoro, kutengeneza, au kusambaza/ kueneza bangi kuwa ukiukaji wa sheria ya serikali ya ushirika. Hata kama mtu asiye raia hajahukumiwa rasmi na au kukubali kutumia bangi, lazima waweze kuonyesha kuwa hawajafanya hatia yoyote

Kufanya Kazi katika Kiwanda cha Bangi

Watu wasio raia wanafaa kufahamu kuwa kufanya kazi kwenye kiwanda cha bangi (katika nyumba za kupandia, zahanati, au vituo vya kipimia) kunaweza kusababisha kunyimwa ombi la ukaaji wa kudumu, kuzuiwa, au kufurushwa. Hii ni pamoja na kazi zinazohusiana na kilimo kama kulengeta, kunyunyizia, kuvuna, pamoja na kazi za kusafisha au kueua vifaa mbali mbali. Kadhalika, Waajiri wanaweza kuwapima dawa za kulevya wafanyikazi wao, na wafanyikazi wanaweza kusimamishwa kazi kwa kosa la kutumia bangi.

Msaada wa Kifedha

Kwa wanafunzi wa kimataifa wanaosoma katika chuo kikuu cha Marekani (hata katika jimbo kama Maine ambalo limehalalisha matumizi ya bangi kwa watu wazima), kutumia bangi ni ukiukaji wa visa yako ya FI.

Upatikanaji wa bangi kwa watoto wenye Uraia wa Marekani kadhalika unaweza kuathiri utafutaji wa elimu ya juu, kwani kufungwa kunaweza kuathiri pakubwa ustahiki wa msaada wa kifedha kutoka kwa serikali ya ushirika . [5]

Rasilimali

Ni Vyema Kujua

Sheria ya Mhamiaji Ya Uhamiaji

Fahamu Haki Zako

Marajeleo

1. National Institute on Drug Abuse. (2021, April 13). What is marijuana? National Institute on Drug Abuse. Iliyoopolewa tarehe 16, Septemba 2021, kutoka kwa https://www.drugabuse.gov/publications/research-reports/marijuana/what-marijuana.

2. National Institute on Drug Abuse. (2021, April 13). How does marijuana produce its effects? National Institute on Drug Abuse. Iliyoopolewa tarehe 16, Septemba 2021, kutoka kwa https://www.drugabuse.gov/publications/research-reports/marijuana/how-does-marijuana-produce-its-effects.

3. Centers for Disease Control and Prevention. (2018, March 16). What you need to know about marijuana use and pregnancy. Centers for Disease Control and Prevention. Iliyoopolewa tarehe 27, Septemba 2021, kutoka kwa https://www.cdc.gov/marijuana/factsheets/pregnancy.htm.

4. What every noncitizen must know about cannabis and immigration. ILRC. (2021, February 26). Iliyoopolewa tarehe 16, Septemba 2021, kutoka kwa https://www.ilrc.org/noncitizens- cannabis-warnings.

5. Get smart about drugs. Federal Student Aid and Consequences of a Drug Conviction |Get Smart About Drugs. (n.d.). Iliyoopolewa tarehe 16, Septemba 2021, kutoka kwa https://www.getsmartaboutdrugs.gov/consequences/federal-student-aid-and-drug-use.

Bangi ni haramu chini Ya Sheria za Marekani.

Watu wasio raia wanaweza kuadhibiwa kwa kutumia au kupatikana na bangi, au kufanya kazi katika kiwanda cha bangi (ikiwa ni pamoja na nyumba za kupandia, zahanati, au vituo vya kupimia). Matumizi ya bangi kwa raia yeyote wa kigeni kunaweza kusababisha kuwekwa kizuizini au kufurushwa kutoka Marekani.

Kituo cha Rasilimali ya Sheria ya Mhamiaji kinapendekeza kuwa wale wasio raia waepukane na bangi katika hali yoyote ile ikiwa ni pamoja na:

- kupatikana na bangi au vikorokoro (karatasi za misokoto, paipu, visagaji) ukiwa nje ya nyumba
- kuchapisha picha zinazohusiana na bangi kwenye mtandao wa kijamii
- kwa mfumo wa picha au video za bangi kwenye simu yako
- ama kuvaa mavazi yaliyo na maneno au nembo ya bangi

Fahamu Haki Zako

Huko Marekani, wale wasio raia wana haki na afisa wa polisi pamoja na Wahusika wa Uhamiaji na Forodha (ICE).

Hizi ni pamoja na:

- Haki ya kuwa kimya
- Haki ya kukataa ridhaa ya kumsaka mtu au mali yako
- Ikiwa utaulizwa maswali na afisa wa uhamiaji au polisi kuhusu ulichonacho au matumizi ya bangi ya hapo awali, usikubali kitu chochote bila kupata ushauri wa mwanasheria

Jifunze Zaidi:

Fahamu Haki Zako

New England (HHS Region 1)
PTTC Prevention Technology Transfer Center Network
Funded by Substance Abuse and Mental Health Services Administration

SAMHSA
Substance Abuse and Mental Health Services Administration